# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
# OFISI YA RAIS,
# TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA

**Kumb.Na KMC/R.30/7/170** **1 Septemba, 2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kupitia wizara ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto imepokea Muongozo wa usimamizi wa maduka ya dawa yanayoendeshwa na vituo vya kutolea huduma za afya kwa Umma, wa Mei 2021.

Hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anawatangazia Watanzania wenye Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi hizo kuanzia tarehe 01 Septemba, 2025.

### 1.0. *MTEKNOLOJIA MSAIDIZI DAWA – NAFASI (04) TGHS A*

Kuajiriwa wenye cheti katika fani ya mteknolojia dawa (pharmaceutical Technologist) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na baraza la pharmacy.

### 1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe Na Elimu ya Kidato Cha Nne Au Kidato Cha Sita, mwenye Astashahada katika Fani ifuatayo:

Pharmaceutical Technologist (Mteknolojia dawa)

### 1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA MSAIDIZI DAWA

(i) Kuandaa mahitaji na matumizi ya dawa na vifaa tiba
(ii) Kuagiza, kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
(iii) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
(iv) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
(v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### 1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali Ya **TGHS A1** kwa mwezi

### 1.0.7 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri wa miaka 18 mpaka 45

ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.

iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.

iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.

v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa

vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.

vii. Waomabji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni

viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.

ix. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 07 Septemba, 2025.

x. ***MUHIMU:*** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe na kutumwa kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
**KAHAMA – Shinyanga.**

xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na

Masudi S. Kibetu
**MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA**
**KAHAMA**

MUNICIPAL DIRECTOR KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL P.O. Box 472 KAHAMA